

## **TAARIFA YA UJENZI WA KITUO CHA MABASI CHA KOROGWE MJINI MRADI WA KUENDELEZA MIJI NA MAJIJI (ULGSP)**

### **1. UTANGULIZI**

Mradi huu wa stendi mpya Kilole ni mradi uliotekelawa na Halmashauri ya Mji Korogwe kwa pesa za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mkandarasi aliyetekelawa mradi huu ni Kampuni ya **NAMIS Corporate Limited** ya Dar-Es-Salaam na Mhandisi Mshauri ni Kampuni ya **NIMETA Consult (T) Ltd** ya Dar-es-Salaam.

Mradi huu ulianza tarehe 15/08/2015 na umekamilika tarehe 30/04/2017 na mkandarasi kukabidhi mradi tarehe 10/05/2017.

Stendi mpya ya Kilole ina maeneo ya maegesho kwa pamoja mabasi **45** yanayoanzia safari katika kituo hiki, eneo la maegesho ya mabasi **15** yanayopitia kituo hiki, eneo la maegesho mabasi madogomadogo ya mjini **33**, eneo la maegesho ya pikipiki (**bodaboda**) **20**, eneo la maegesho ya bajaji **28**, eneo la maegesho ya *taxis* **14**, eneo la maegesho ya magari **14** ya watu binafsi, eneo la maegesho ya magari ya polisi, eneo la maegesho magari **15** ya waenda madukani na eneo la maegesho magari **16** ya watu binafsi wanaokuja kukata tiketi.



**Jengo la Abiria kusubilia usafiri**

Pamoja na hayo, kuna maduka **122** yanayounda sehemu ya uzio pamoja na vyoo vyake, kuna jengo la utawala, choo cha wasafiri chenye matundu **5** kwa wanawake na **5** kwa wanaume, pamoja na tundu moja moja kwa walemavu kwa jinsia zote, jengo la abiria ambalo lina mgahawa na duka la kisasa (super market), ofisi za kukatia tiketi 27, kituo kidogo cha polisi, vibanda vya walinzi getini **2**, na Traffic check point ofisi 1 pamoja na huduma za ATM (zitawekwa). Pia

kuna barabara za ndani na nje ya kituo pamoja na mifereji ya maji ya mvua. Aidha Mkurugenzi wa Mji amekwishamteua mionganini mwa watumishi Meneja wa mradi pamoja na wasaidizi wake wawili ili kusimamia shughuli za utawala na uendeshaji. Utaratibu wa kugawa maeneo ya kufanya biashara kwa waliiomba upo katika hatua ya kuwasilishwa katika kikao cha kamati kupata baraka.



**Vibanda vinavyozunguka kama uzio wa stendi**

## **2. GHARAMA ZA MRADI**

Mradi huu umetekelizwa kwa jumla ya pesa za Kitanzania bila VAT shilingi bilioni nne, milioni ishirini na tatu, laki mbili arobaini na tano elfu, mia nne na moja na senti thelathini na saba tu (4,023,245,401.37). Mhandisi Mshauri NIMETA Consult (T) Ltd anatekeleza kazi ya usanifu, ushauri na usimamizi kwa jumla ya pesa za Kitanzania bila VAT milioni mia tisa arobaini na saba na laki mbili tu (947,200,000) kwa usimamizi wa miradi mitatu ambapo awamu ya kwanza ni Kituo kipycha cha mabasi Kilole.

## **3. FAIDA ZA MRADI**

Mradi huu mkubwa ambao kuwepo kwake kumewezesha, Kuwepo kwa mazingira mazuri na salama kwa Wasafiri na Wasafirishaji, kuongezeka kwa ajira kwa wakazi wa Korogwe na maeneo ya jirani, ambapo majengo na miundombinu iliyopo katika stendi inategemewa kutoa

ajira kwa watu **360** na shughuli nyinginezo kwa watu takribani **150**, Kuongeza uwekezaji kwa wafanyabiashara. Kuongezeka kwa mapato ya ndani ya Halmashauri zaidi ya Shilingi milioni mia tatu kwa mwaka na mapato mengine ya Serikali kuu.



#### **Ofisi za kukatia tiketi**

#### **5. CHANGAMOTO**

Suala la msamaha wa kodi (**VAT Exemption**) ni tatizo kubwa ambalo lipo kwenye mradi huu, ambapo imekuwa ni ngumu kuupata msamaha kutokana na kwamba ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na Wizara ya fedha bado wapo kwenye mazungumzo. Aidha, kukosekana kwa msamaha huu wa kodi utasababisha Halmashauri kulipa deni hili kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani.

**Jumanne K. Shauri  
MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI KOROGWE**